

Tunafurahia hali ya hewa na hali ya maisha nzuri hapa Queensland. Hata hivyo, majanga ya kimaumbile kama vile tufani, dhoruba, na mafuriko, ni sehemu tusiyoepekika nayo katika mazingira yetu. Historia imeonyesha kwamba hatuwezi kunyamaza kuhusu hatari zinazoletwa na haya.

Chukua muda sasa na ujitayarishie dharura kwa:

- Kutayarisha Mpango wako wa Dharura
- Kutayarisha Mkoba wako wa Dharura,
- Tayarisha nyumbani pako; na
- Sikiliza onyo zitakazotolewa.

Hatua hizi rahisi zinaweza kukusaidia kujitayarishia, kuokoka, na kupunguza athari ya majanga ya kimaumbile.

Muda bora zaidi wa kuchukua hatua na kutayarisha nyumbani pako ni kabla ya msimu wa dhoruba, tufani na masika.

Zifuatazo ni anuwai ya kazi pendekezwa za kukusaidia katika kujitayarisha nyumbani pako na mahali unapomiliki ili kupunguza uwezekano wa madhara.

1. Ukarabati wa kawaida wa nyumbani

- Angalia hali ya paa na tengeneza vigae vilivyolegea, mabati na hata skrubu za paa;
- Safisha mifereji na mabomba ya kuteremsha maji ili maji yaweze kuteremka kwa haraka iwezekanavyo;
- Punguza miti na matawi yanayoning'inia (tahadhari na nyaya zozote za umeme zinazopita juu); na
- Salimisha vitu vilivyolegea karibu karibu na mali yako na bustani ambavyo vinaweza kusababisha madhara kama vitapeperushwa na upepo mkali (kama vile fenicha ya bustani na wanasesere)

2. Matayarisho ya kawaida ya nyumbani

- Hakikisha kuwa bima yote ya nyumbani pako, yaliyomo na ya gari iko sawa na inawekeka bima mali yako kwa utoshelevu – angalia kama sera yako inajumuisha usafishaji wa uchafu pamoja na kutupwa kwake;
- Tambua ni chumba kipi ambacho ni sehemu ya nguvu zaidi ya nyumbani, ikiwa unahitaji kujikinga nyumbani pako wakati wa dhoruba kali au tufani. Kawaida hiki kitakuwa chumba kidogo zaidi katika nyumba, na kilicho na madirisha machache zaidi;
- Tambua ni wapi ambapo na jinsi unavyoweza kuzima mfereji mkuu wa maji, umeme na gesi;
- Tahadhari na taratibu zozote za kuzimwa zitokazo kwa mtengenezaji za mifumo ya umeme ya sola; na
- Nunua vitu muhimu vya dharura vinavyoweza kusaidia kama vile:
 - mikebe ya kuhifadhi maji ya kutumiwa,
 - mafuta ya ziada kwa matumizi katika gari lako (hakikisha kwamba unayahifadhi kwa usalama),
 - Tepu pana ya masking ya kutoshea kwenye madirisha, na
 - mabegi ya gunia na mchanga wa kuweka kwenye mabegi kwenye mifereji ya ndani ya kuzuia maji taka yanaweza kurushwa na mafuriko.

3. Kama unaishi katika eneo la kuelekea mafuriko:

- Hifadhi sumu zote katika kiwango cha juu zaidi kutoka kwenye ardhi endapo kutakuwa na mafuriko ya ghafla
- Tambua ni vitu vipi vya nyumba

utakavyohitaji kupandisha juu au kupunguza kama mafuriko yatatishia nyumbani pako; na

- Fikiria yafuatayo:
 - mbadala wa kufunika sakafu kwa zulia,
 - kubadilisha soketi ya umeme na sehemu za umeme na kuziweka juu zaidi katika kiwango kilicho mbali na sakafu, kwa kutumia mtoaji huduma aliyeidhinishwa kwa maswala ya umeme.

4. Kama unaishi katika eneo linalokumbwa na tufani au dhoruba kali:

- Weka madirisha yaliyo na vilango au skrini za chuma kwa ulinzi wa ziada wakati wa upepo mkali; na
- Weka mpango kupata mjengaji wa utaalamu wa kuweza kuangalia jengo lako na kutambua maswala yanayohitajika katika kuongeza usalama wa kimuundo nyumba yako kuweza kuhimili upepo mkali.

5. Wakati onyo za hali ya hewa za tufani au dhoruba kali zinapotolewa:

- Ondoa kwenye umeme vifaa vyote vya umeme pamoja na vinaso mawimbi vyote vya nje vya televisheni na radio;

- Zima sehemu zote kuu kunakotokea umeme na gesi kama utaelekezwa na wahusika wa dharura;
- Salimisha fenicha zote ziko nje pamoja na vitu vingine vya bustani;
- Jaza ndoo pamoja na bafu kwa maji safi endapo kutakuwa na hitilafu ya mfereji mkuu wa maji;
- Funga madirisha yaliyo na vilango au weka tepu kwenye madirisha katika ruwaza ya kuingamana kwa kutumia tepu thabiti na uvute pazia;
- Egeza magari chini ya paa, mbali na miti, nyaya za umeme na njia za kupita maji;
- Kama huwezi kufikia sehemu ya kufunika gari lako, lisalimishe kwa nguvu na blanketi zilizofungwa ili kupunguza uharibifu wa mawe ya theluji;
- Angalia na uhakikishe kuwa wanafamilia wote wako salama na wamejikinga katika chumba cha thabiti zaidi kwenye nyumba; na
- Chukua Mfuko wako wa Dharura na uingie nao huko huku unapojikinga na dhoruba au tufani; na
- Sikiliza kituo chako kilicho karibu cha radio kwa maelezo kuhusu kinachojiri pamoja na onyo za ziada na ujumbe wa usalama.

siku zote kumbuka

Kutayarisha nyumbani pako ni hatua muhimu katika kuifaa familia yako katika kujitayarisha kwake, kuokoka na kuweza kudhibiti na dharura zilizopo.

Broshua hii ni kwa taarifa pekee na imetolewa kwa roho safi. Idara ya Usalama wa Jumua, Usimamizi wa Dharura wa Queensland na Huduma ya Dharura ya Serikali yote haitawajibikia mtu yeyote kwa mujibu wa kupoteza au kuharibika kokote (kukiwemo athari ya kupoteza au kuharibu) ambayo kunaweza kupatikana au kutozwa, au kunakoweza kutokea moja kwa moja au vinginevyo, kwa mujibu wa kutegemea wa mtu yeyote katika taarifa ilimo kwenye broshua hii.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kujitayarishia kwa dharura tembelea www.disaster.qld.gov.au